

# Hati ya Uhuishaji

**Je, upatikanaji wa umeme unaathiri vipi raia nchini Kenya?**

Dkt. Elizabeth Baldwin, Dkt. Jennifer Brass, Dkt. Christopher Gore, Dkt. Lauren MacLean, Dkt. Winnie Mitullah na Dkt. Alesha Porisky

**Ili kunufaika zaidi na hati hii, unaweza:**

- Kuibandika kwenye daftari lako kama kumbukumbu ya kuangalia uhuishaji wa timu.
- Kuisimamisha uhuishaji kwa muda na andika vidokezo kadri unavyoendelea.
- Kuongeza vielelezo vyako mwenyewe kwenye karatasi.
- Kuengeneza uhuishaji wako mwenyewe kuambatanisha na huu.
- Kuongeza maelezo kutoka kwenye majadiliano ya darasani.
- Kuweka kumbukumbu ya maeneo ambayo utayachunguza zaidi.
- Kuandika kumbukumbu ya maneno muhimu na ufafanuzi.
- Kuongeza maswali ambayo ungependa yajibiwe - unaweza kutuma ujumbe kwa wanachama wa timu kupitia kisanduku cha maoni kilicho chini ya makala yao: **futurumcareers.com/how-does-access-to-electricity-impact-citizens-in-kenya**

## HATI:

Kenya inaongoza duniani kwa nishati ya kijani, na zaidi ya 90% ya umeme wake unatokana na vyanzo mbadala. Kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, asilimia ya nyumba zinazopata umeme imeongezeka maradufu hadi karibu 80%. Haya ni mafanikio makubwa, lakini bado kuna changamoto nyingi za kupatikana umeme miongoni mwa Wakenya.

Shida mojawapo ni kwamba usambazaji wa umeme sio wa kutegemewa kwa hivyo kukatika kwa umeme ni jambo la kawaida. Pia kutumia umeme ni ghali. Wasiwasi mwingine ni kwamba sio Wakenya wote walio na aina sawa ya umeme. Wakati baadhi wameunganishwa kwenye gridi ya taifa, wengine wanategemea tu nishati ya jua. Wakati mwingine 'kuwa na umeme' nchini Kenya kunamaanisha kuwa na paneli ndogo ya jua ambayo inaweza kuwasha balbu na kuchaji simu pekee.

Timu ya kimataifa ya watafiti kutoka Kenya, Kanada, na Marekani inachunguza changamoto za kuongeza upatikanaji wa umeme nchini Kenya na athari kwa uchumi, jamii na siasa.

Timu ilifanya tafiti na nyumba kote nchini. Waliuliza ni aina gani ya umeme ambayo watu wanayo, ni ya kutegemewa kwa kiasi gani, inagharimu kiasi gani na jinsi gani inabadilisha maisha yao ya kila siku. Timu ilikutana na raia wa Kenya katika jamii ndogo  vijijini na kaytika miji mikubwa ili kupata uelewa wa kina kuhusu uzoefu wao. Pia waliwahoji watumishi wa umma, wanasiasa, wamiliki wa biashara na mashirika ya kimataifa kuhusu sera za umeme.

# Hati ya uhuishaji

Changamoto moja kuu ya kuongeza upatikanaji wa umeme nchini Kenya ni gharama. Ni ghali sana kwa serikali kupanua gridi ya taifa kumfikia kila mtu, hasa katika maeneo ya vijijini. Pia ni ghali kwa Wakenya kuunganisha nyumba au biashara zao na gridi ya taifa. Pia gharama ya kutumia umeme wakati ni kubwa sana nchini Kenya, haswa ikilinganishwa na nchi zingine. Nyumba ambazo hazijaunganishwa na gridi ya taifa mara nyingi huwa na paneli ndogo tu za jua, na watu wengi hushindwa kumudu malipo.

Hii ina maana kwamba ingawa asilimia kubwa ya nyumba na wafanyabiashara wa Kenya wanachukuliwa wanapata umeme, ukweli ni kwamba watu wengi hawawezi kumudu umeme wa kutosha kukidhi mahitaji yao. Aidha, kwa wale walio na umeme, upatikanaji wake sio wa kutegemewa.

Licha ya changamoto hizi, faida ya kupata umeme kwa Wakenya ni kubwa. Wakati wa utafiti, Wakenya walizungumzia jinsi umeme ulivyoimarisha usalama wao wa kibinafsi usiku na kuwasaidia katika biashara zao. Kutumia umeme kuliwawezesha watoto kusoma kwa muda mrefu na kuboresha afya kwani watu waliacha kutumia taa chafu za mafuta ya taa. Upatikanaji wa habari uliboreshwa na wakati mwingine watu walitumia mitandao ya kijamii, kama vile WhatsApp, ili kuwafikia wanasiasa. Manufaa yanayoweza kupatikana kutokana na kupata umeme ni makubwa. Hii inamaanisha kwamba wale wenye umeme wako katika hali nzuri zaidi kuliko wale wasiokuwa nao.

Ikiwa Kenya inaweza kuendeleza mafanikio yake ya nishati ya kijani na kuboresha kutegemewa na uwezo wa kumudu umeme, basi maisha ya wananchi wengi yataboreshwa sana.

Una maswali gani kuhusu upatikanaji wa umeme nchini Kenya?